# JARIDA LA HABARI

ISO: 90012015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga


Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

TOLEO NAMBA: 005 JUNI, 2020 www.meteo.go.tz


## MSIMU WA KIPUPWE: UPEPO MKALI NA BARIDI

"Msimu huu wa kipupwe unatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya upepo mkali wa kusi na hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nchi hata hivyo, vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini-magharibi husuan nyakati za usiku na asubuhi". Alisema Dkt. Kijazi

uk.4




## MSAJILI WA HAZINA AAGIZA TMA KUCHANGIA MFUKO WA SERIKALI KUPITIA UKUSANYAJI WA MAPATO

"Kupitia Ofisi yangu tutaendelea kuwasaidia na kuwapa ushirikiano katika kutimiza majukumu yenu mapya mliyokasimiwa kisheria. Aidha, nawakumbusha jukumu kubwa la kuongeza mapato na kuchangia katika mfuko wa serikali". Alisema Bw. Mbuttuka

uk.9



# BODI YA TMA YAKAGUA MRADI WA RADA - MTWARA






# BODI YA TMA YAKAGUA MRADI WA RADA YA HALI YA HEWA MTWARA



*Wajumbe wa bodi ya TMA wakipata maelezo kutoka kwa Mkandarasi wakati wa ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa rada ya hali ya hewa mkoani Mtwara.*

Mtwara;

Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imefanya ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa mradi wa Rada ya hali ya hewa unaogharimu kiasi cha zaidi ya Tsh. Bilioni 6, rada hiyo inayotarajiwa kufungwa katika kilima cha Mbae, Mtwara, ambapo utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 80 na kuleta maendeleo mbalimbali ikiwemo miundombinu ya barabara, maji na umeme kwa kaya zaidi ya 750 za Mtaa wa Mbae 'A'.

Akizungumza baada ya kukagua majengo ya eneo hilo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dkt. Buruhani Nyenzi kutoka Dar es Salaam alimtaka mkandarasi ahakikishe anamaliza sehemu iliyobaki kulingana na makubaliano ya mkataba pamoja na kuwa imetokea changamoto ya COVID 19 iliyopelekea wataalamu wanaotakiwa kuja kuifunga rada hiyo kutoka Marekani kushindwa kufanya hivyo.

Aidha, aliishukuru Serikali kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya Rada hiyo kwa vile itakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wa mikoa ya Kusini, huku akiomba uongozi wa mkoa wa Mtwara kuhakikisha eneo la Rada linakuwa salama wakati wote.

"Ningeomba sana uongozi wa mkoa wajaribu kuangalia barabara isiharibike, hili ni tatizo ambalo nimeliona sehemu nyingine, barabara kama hii imetengenezwa baada ya muda unakuta imeharibika kwa sababu ya kukosa usimamizi wa kutosha kutoka katika uongozi wa eneo husika". Alizungumza Dkt. Nyenzi

Kwa upande mwingine, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt. Makame Omar Makame kutoka Zanzibar alielezea shukrani zake kwa serikali kwa vile umuhimu wa rada hiyo ni kwa manufaa ya nchi nzima kwa vile taarifa zitazopatikana zitasaidia maendeleo ya nchi katika sekta mbalimbali kama vile usafiri wa baharini, nchi kavu, uvivu, kilimo n.k

"Rada hii ni muhimu kwa mwambao wa bahari ikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba lakini pia katika mwambao wa Dar es Salaam mpaka kufikia Mtwara, hivyo kumalizika kwake kutatoa fursa ya kupata taarifa zenye usahihi wa utabiri wa hali ya hewa kwa shughuli mbalimbali". Aliongezea Dkt. Makame.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TMA na makamu wa tatu wa rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani, Dkt. Agnes Kijazi aliishukuru Bodi hiyo kwa kutembelea eneo la Rada na pia aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa nchini. Alieleza kuwa, ufungwaji wa rada hiyo utasaidia wananchi wa mikoa ya kusini kupata taarifa sahihi kwa vile ina uwezo wa kuona maeneo madogomadogo zaidi na kuweza kutambua aina ya mvua, eneo mvua inaponyesha, kuona matone ya mvua, vimbunga na hivyo kusaidia kuboresha utabiri kwa ujumla.

"Serikali imekwisha kulipia rada mbili ambazo zitafungwa Mbeya na Kigoma, hapo utaona katika mtandao wa rada ukijumuisha Dar es Salaam, Mwanza na hii ya Mtwara utakuwa umefikia rada tano lakini matarajio yetu ni kuwa na rada saba nchini, tayari Mamlaka imekwisha kutengewa bajeti katika mwaka wa fedha 2020/21 ya kufunga rada mbili za Dodoma na Kilimanjaro, hivyo kufikia mwaka ujao wa fedha, Mamlaka itakuwa imekamilisha idadi ya rada saba zinazohitajika nchini". Aliongeza Dkt. Kijazi.


Aliendelea kwa kuelezea vifaa vyote vya rada vimekwishafika na kwamba wanasubiriwa wataalamu kutoka Marekani ambao wamekwama kutokana na janga la COVID 19, vile vile alieleza kuwa eneo hilo la ujenzi limejumuisha jengo la mtambo, jengo la wataalamu, jengo la mlinzi, ukuta na mnara utakaoshika antenna ya rada. Kwa upande wa namna TMA ilivyojipanga, Dkt. Kijazi alisema tayari waatalam wa ndani wamepatiwa mafunzo ikiwa na kufanikiwa kufika mpaka kiwandani, hivyo kazi iliyobakia ni kuleta matokea chanya kwa maendeleo ya nchi.

Ziara ya Bodi hiyo ilifanikiwa pia kwa kutembelea ofisi ya TMA Kanda-Mtwara na kujionea shughuli za Ofisi hiyo pamoja na kupata taarifa fupi ya Kanda kutoka kwa Meneja wa Kanda hiyo Ndugu. Amas Daudi.

JARIDA LA HABARI
ISO: 90012015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga   Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

**Jarida hili limeandaliwa na**
**Mhariri -** Dkt. Agnes Kijazi
**Mwandishi -** Monica Mutoni , **Msanifu Kurasa -** Byats Bavuga

# DKT. KIJAZI: MWAKA 2019 ULIREKODI KIASI CHA MVUA NYINGI TANGU MWAKA 1970







*Dkt. Agnes Kijazi Mkurugenzi Mkuu waTMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO)*

Dar Es Salam;

M ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa ripoti ya tathimini ya hali ya hewa ya Tanzania kwa mwaka 2019. Uzinduzi wa ripoti hiyo ulifanyika wakati wa kikao cha Bodi ya TMA kilichofanyika katika ofisi za Makao Makuu ya TMA.

Akizungumzia ripoti hiyo Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Agnes Kijazi alisema mwaka 2019 umechukua nafasi ya nne kwa kurekodi kiasi cha mvua nyingi tangu mwaka 1970.

"Kiwango cha mvua nchini kwa mwaka 2019 kilikuwa ni wastani wa milimita 1283.5 sawa na asilimia 125 ya wastani wa mvua ya muda mrefu (1981-2010), kiwango hiki ni zaidi ya wastani wa mvua ya muda mrefu kwa milimita 256.5. Katika historia, mvua hii imechukua nafasi ya nne kwa wingi kati ya miaka iliyopata mvua nyingi zaidi tangu mwaka 1970 ambapo miaka iliyokua na mvua nyingi zaidi tangu mwaka 1970 ni 1982, 1997 na 2006". Alisema Dkt. Kijazi


Aidha, ripoti hiyo ilieleza kuwa takwimu zinaonesha kuwa joto la nchi limeendelea kuongezeka kwa kiwango cha juu kuanzia mwaka 1995, ambapo joto la usiku limeongezeka zaidi ilikilinganishwa na joto la mchana. Pamoja na hayo taarifa za ripoti zitolewazo zimekuwa zikichangia ripoti za tathimini ya hali ya hewa ya dunia zinazoandaliwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Vilevile Dkt. Kijazi alitoa wito kwa wadau wa sekta mbalimbali kutumia taarifa zilizopo kwenye ripoti hiyo kwaajili ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi na jamii kama vile kilimo, ujenzi, maendeleo ya viwanda n.k

Awali wakati akitoa maelezo ya jumla, Mkurugenzi wa Utafiti na Matumizi ya Hali ya Hewa, Dkt. Ladislaus Chang'a alisema kuwa, ripoti hizi zimekuwa zikitolewa tokea mwaka 2011 hadi 2019 na lengo ni kukuza ufahamu na uelewa kwa jamii, wadau na watoa maamuzi juu ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi. "Tathmini za ripoti hizi huonesha taarifa za kina za uchambuzi wa hali ya hewa na athari zake na kuziweka katika mtazamo wa kihistoria". Alisema Dkt. Chang'a

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Dkt. Buruhani Nyenzi alipongeza Menejimenti ya TMA kwa kutoa taarifa hiyo kwani ilielezwa kwamba ni nchi mbili tu Afrika ambazo zinatoa taarifa hizo ikiwemo Tanzania na Ivory Coast.

# MSIMU WA KIPUPWE: UPEPO MKALI NA BARIDI




Dar Es Salam;

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa rasmi mwelekeo wa hali ya hewa wa msimu wa kipupwe hapa nchini, unaoanzia Mwezi Juni – Agosti 2020, taarifa hiyo imeelezea athari zinazoweza kujitokeza pamoja na ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akizungumzia msimu huo, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi aliwataka wananchi kufuatilia utabiri huo wa msimu wa kipupwe kwa kipindi cha Juni-Agosti (JJA) 2020, ambapo mvua za msimu wa Machi hadi Mei ambazo zilileta athari hapa nchini zimeisha.

“Msimu huu wa kipupwe unatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya upepo mkali wa kusi na hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nchi hata hivyo, vipindi vya baridi kali vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini-magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi”. Alisema Dkt. Kijazi

“Vipindi vya baridi kali vinatarajiwa hasa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Juni na kupungua kuelekea mwishoni mwa msimu yaani mwezi Agosti kwa maeneo ya mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Rukwa pamoja na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Ruvuma, maeneo haya yanatarajiwa yatakuwa na joto la kawaida kati ya nyuzi joto 6 na 12, hata hivyo baadhi ya maeneo hususan katika mikoa ya Njombe na Mbeya yanatarajiwa kuwa na joto la chini ya nyuzi joto 6”. Aliongezea Dkt. Kijazi

“Nawakumbusha wananchi kuchukua tahadhari na kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania”, alisisitiza Dkt. Kijazi

Akitoa ufafanuzi zaidi, Dkt. Kijazi alielezea hali ya joto katika maeneo mengi hapa nchini, huku akibainisha kuwa joto la kawaida linatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa Pwani na kuashiria uwepo wa vipindi vichache vya baridi ikilinganishwa na hali ya wastani wa muda mrefu (1981-2010) kwa miezi ya Juni-Agosti katika maeneo hayo.

Akizungumzia kuhusu mvua, Dkt. Kijazi alisema, vipindi vya Upepo unaovuma kutoka mashariki na kusini mashariki (Matlai) vinatarajiwa kuleta unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi na kusababisha kuwepo na matarajio ya vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Akizungumzia athari zinazoweza kujitokeza, Dkt. Kijazi alisema, hali ya ukavu na upepo inaweza kuongeza upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo na kuathiri upatikanaji wa maji kwa mazao, mifugo na matumizi mengine. Jamii inashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

“Jamii inashauriwa kuzingatia matumizi endelevu ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza, wakati huohuo wakizingatia tahadhari za upepo mkali ambazo zitaendelea kutolewa na TMA kila upepo mkali utakapojitokeza”. Alimalizia Dkt. Kijazi.

# TMA KUWA MSTARI WA MBELE KUSAIDIA HUDUMA ZA HALI YA HEWA KATIKA NCHI ZA AFRIKA



*Picha 1:Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi akichangia katika taarifa ya utekelezaji wa shughuli za WMO katika Kanda ya Afrika (RA I) iliyowasilishwa na Katibu Mkuu wa WMO, Prof. Petteri Taalas katika Mkutano wa viongozi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Kanda ya Afrika (WMO Regional Association I Management Group) uliofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 10 hadi 12 Juni 2020.*



*Picha 2:Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Kanda ya Afrika, Dkt. Daouda Konate (kushoto aliyevaa miwani) aliyekuwa Mwenyekiti wa Kikao akimsikiliza Katibu Mkuu wa WMO, Prof. Petteri Taalas (kushoto aliyekaa katikati ya wataalamu) akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za WMO katika Kanda ya Afrika (RA I) katika Mkutano wa viongozi wa WMO Kanda ya Afrika (WMO Regional Association I Management Group) uliofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 10 hadi 12 Juni 2020.*

Dar Es Salam;

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema iko tayari kushirikiana na Taasisi za Hali ya Hewa za Nchi Wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Kanda ya Afrika (WMO Regional Association I (RA I), kusaidia kuboresha huduma za hali ya hewa katika maeneo ambayo imekwisha kupiga hatua zaidi. Hayo yalisemwa katika Mkutano wa Viongozi wa WMO Kanda ya Afrika (RA I Management Group), uliofanyika kwa njia ya mtandao (videoconference) kuanzia tarehe 10 hadi 12 Juni, 2020.

Akizungumza wakati akichangia taarifa ya utekelezaji wa shughuli za WMO katika Kanda ya Afrika iliyowasilishwa na Katibu Mkuu wa WMO Prof. Petteri Taalas, Mkurugenzi Mkuu wa TMA ambaye pia ni Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi alieleza kwamba Tanzania imepiga hatua katika uandaaji wa majarida ya taarifa za klaimatolojia (hali ya hewa ya muda mrefu) kwa nchi ya Tanzania, hivyo iko tayari kusaidia nchi nyingine Wanachama wa WMO Kanda ya Afrika.

"Kuhusiana na uandaaji wa taarifa za klaimatolojia (hali ya hewa ya muda mrefu), nafurahi kusema kwamba Tanzania tumekwishaanza kutoa machapisho hayo tangu mwaka 2011 na tuko tayari kusaidia katika ngazi ya Kanda". Alisema Dkt. Kijazi".

Aidha, aliendelea kusisitiza utayari wa Tanzania katika kusaidia nchi zingine wakati akielezea faidi za kuwa na Mfumo wa Kitaifa wa Huduma za Hali ya Hewa (National Framework for Climate Services) ambapo alisema kwa upande wa Tanzania, mfumo huo umesaidia kuboresha sana huduma za hali ya hewa. Moja ya uboreshaji huo ni kutungwa kwa sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Na. 2 ya mwaka 2019 ambayo ina malengo ya kuiwezesha TMA kusimamia vyema huduma zote za hali ya hewa zinazotolewa nchini Tanzania na hivyo kutekeleza vyema program zote za WMO kwa ustawi wa wananchi wa Tanzania na dunia kwa ujumla hasa ikizingatiwa kwamba hali ya hewa haina mipaka. Aliongeza Dr. Kijazi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa WMO alimpongeza Dkt. Kijazi kwa umahiri anaoonyesha katika kushiriki kwenye program za WMO katika nafasi yake kama Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani na kama Makamu wa Tatu wa Rais wa shirika hilo. Aidha, aliipongeza Tanzania kuwa imefanya kazi kubwa katika kutekeleza program za WMO ikiwemo program ya Global Framework for Climate services na akasema WMO inafurahishwa na utayari wa Tanzania kusaidia nchi zingine barani Afrika.

Kwa upande mwingine, Mkurugenzi wa WMO Ofisi ya Kanda ya Afrika, Dkt. Amos Makarau alitoa taarifa ya wataalamu walioteuliwa kuongoza majopo na vikosi kazi mbalimbali vya WMO, ambapo taarifa hiyo ilibainisha uteuzi wa Mkurugenzi wa Miundombinu na Huduma za Ufundi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Dkt. Pascal Waniha kuwa Makamu Mwenyekiti (Vice Chair) wa Kikosi Kazi cha Mtandao wa Dunia wa Upimaji wa Hali ya Hewa (Study Group on Global Basic Observing Network (GBON), akiwa miongoni mwa wataalamu watatu (3) walioteuliwa kutoka Afrika kuongoza majopo na vikosi kazi vya WMO. Hii ni sifa na heshima kwa Tanzania na TMA.

Awali akifungua mkutano huo, Mwenyekiti ambaye ni Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Kanda ya Afrika, Dkt. Daouda Konate kutoka Ivory Coast alisema lengo la mkutano ni kujadili utekelezaji wa shughuli za huduma za hali ya hewa katika Kanda ya Afrika. Mkutano ulijadili masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na shughuli za WMO katika Kanda ya Afrika; utekelezaji wa maazimio ya Mkutano Mkuu wa WMO (WMO Congress) wa mwezi Juni, 2019; Uteuzi wa wataalamu katika majopo na vikosikazi vya WMO; Vipaumbele vya Kanda; Mpango Mkakati wa Kanda; na athari za janga la ugonjwa wa "COVID-19" katika huduma za hali ya hewa.

Aidha, baada ya majidiliano ya kina, mkutano ulikuja na mapendekezo ambayo ni pamoja na: kutoa nafasi kwa watunga sera kushiriki katika mikutano ya Kanda ya Masuala ya hali ya hewa; na kuziomba Nchi Wanachama kuridhia katiba ya Kamati ya Mawaziri wenye dhamana ya hali ya hewa "African Ministerial Conference on Meteorology (AMCOMET).

# TANZANIA YAONGOZA MKUTANO WA KUWIANISHA SHUGHULI ZA UTOAJI HUDUMA ZA HALI YA HEWA KATIKA UKANDA WA SADC



*Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa WMO, Dkt. Agnes Kijazi akijibu hoja za wajumbe wa mkutano wa SADC Sekta ya Hali ya Hewa. Aliyekaa kulia kwake ni Meneja Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa wa TMA, Bw. Wibert Muruke akiandika muhtasari wa kikao.*


*Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa WMO, Dkt. Agnes Kijazi akiongoza Mkutano wa SADC Sekta ya Hali ya Hewa uliofanyika kwa njia ya mtandao katika katika kituo cha kimataifa cha mikutano cha Mwalimu Julius Nyerere (JNICC), Jijini, Dar es Salaam. Aliyekaa kulia kwake ni Meneja Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa wa TMA, Bw. Wibert Muruke akifuatilia majadiliano ya kikao.*

Dar Es Salam;

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi amesisitiza kwamba suala la kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa wanaotoa huduma kwa watumiaji wa bahari ni la umuhimu wa kipekee ili kuweza kukidhi mahitaji ya wadau hao wa bahari.

Amezungumza hayo wakati akishiriki katika mkutano wa Bodi ya Mashirikiano kati ya WMO na Kamisheni ya Kimataifa ya Masuala ya Huduma za Hali ya Hewa kwa watumiaji wa Bahari (WMO-Intergovernmental Oceanographic Commission Collaborative Board (WMO-IOC JCB)) uliofanyika tarehe 16 Juni, 2020 kwa njia ya mtandao (videoconference).


“Taasisi nyingi za Hali ya Hewa zina vituo vya kufuatilia hali ya bahari na kutoa huduma kwa wadau, lakini wataalamu bado hawajapewa ujuzi wa kutosha kuhusiana na mahitaji ya wadau. Hivyo tunahitaji kushughulikia masuala muhimu ya kisera na kimkakati yatakayowezesha kujenga uwezo kwa wataalamu katika ngazi ya nchi,”. Alisema Dkt. Kijazi.

Aidha, Dkt. Kijazi alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuimarishwa kwa miundombinu ya upimaji na ufuatiliaji katika maeneo ya bahari ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu ambazo ni muhimu katika utoaji wa huduma katika sekta hii, pamoja na ushirikiano kati ya taasisi husika kuanzia ngazi ya nchi.

Bodi ya mashirikiano katika ya WMO na IOC (WMO-IOC Joint Collaborative Board) huratibu maeneo ya mashirikiano kati ya WMO na IOC, na kwa sasa pamoja na masuala mengine itashughulikia pia suala la kujenga uwezo katika maeneo ya mashirikiano. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja rasimu ya mkakati wa miaka kumi (10) wa kujenga uwezo, ambao utahusisha utaratibu wa kufanya kazi pamoja; utaratibu wa kushirikiana na washirika wengine; na uendelevu katika shughuli za kujenga uwezo.

Bodi hiyo ilikutana kwa lengo la kujadili vipaumbele vya maeneo ya ushirikiano yanayohitaji kujengewa uwezo, ambayo yatashughulikiwa na majopo ya kujenga uwezo ya WMO na IOC. Dkt. Kijazi ni Mwenyekiti wa Jopo la WMO la kujenga uwezo (WMO Capacity Development Panel).

# MHE. NDITIYE AAGIZA BARAZA LA TMA KUANDAA MIONGOZO NA MAFANIKO YENYE TIJA KWA SERIKALI




*Mhe. Mhandisi. Atashasta Nditiye Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, akihutubia Baraza la Wafanyakazi wa TMA, lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020. Tarehe 16 na 17 Machi, 2020.*

Dodoma;

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Mhandisi. Atashasta Nditiye ameagiza wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuandaa miongozo na mafanikio yenye tija kwa Mamlaka na Serikali kupitia mijadala ya Baraza hilo.

Mhe. Mhandisi. Nditiye alitoa maagizo hayo wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) linalofanyika katika Ukumbi wa Takwimu, Dodoma, Tarehe 16 na 17 Machi 2020.

"Hakikisheni kwamba mnaweka vyema vipaumbele vyenu, na kutimiza mambo ya msingi kwanza ili kukabiliana na tatizo la ufinyu wa bajeti lililopo". Alisema Mhe. Mhandisi. Nditiye

Aidha Mhe. Naibu Waziri aliitaka Mamlaka kuharakisha upatikanaji wa kanuni ili sheria ianze kufanya kazi kurahisisha ufanisi wa majukumu ya Mamlaka.

"Endeleeni kuboresha utabiri na kutoa tahadhari za hali mbaya ya hewa kwa wakati na kwa usahihi kwa jamii ya watanzania na wageni wanaotembelea nchini, kwa kusema hivi naamini michango yenu katika mkutano huu wa Baraza lenu la wafanyakazi, itatoa matokeo makubwa yatakayoendeleza sekta ya hali ya hewa nchini na pia kuliwezesha Taifa letu kusonga mbele kiuchumi na kimaendeleo". Alisisitiza Mhe. Mhandsi. Nditiye.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi alimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kujumuika na wajumbe wa Baraza katika ufunguzi wa Baraza hilo na Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa iliyoonesha katika kuboresha muundo mpya wa Mamlaka unaolenga kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

"Uwepo wako umetupa nguvu na ari mpya katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi hasa katika kipindi hiki ambacho TMA imekuwa Mamlaka kamili".Alieleza Dkt. Kijazi

Aliendelea kwa kumueleza kuwa Baraza la mwaka huu ni kwa mujibu wa mkataba mpya kati ya Menejiment na TUGHE na linajumuisha wajumbe 98 kutoka vituo mbali mbali vya hali ya hewa hapa nchini ikijumuisha viongozi na wawakilishi wa wafanyakazi.


Kwa upande wake mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Bi Jane Kikunya alimuomba Mhe. Naibu Waziri kusaidia katika kutatua changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa kuongeza zaidi bajeti kwaajili ya kusaidia uboreshaji wa vifaa vya hali ya hewa

Mkutano huo wa Baraza ulianza na elimu ya namna ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Korona katika maeneo yao ya kazi na jamii kwa ujumla.




*Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la TMA katika picha ya pamoja na mgeni Rasmi Mhe. Mhandisi. Atashasta Nditiye katika baraza hilo lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020.*

# MKURUGENZI MKUU TMA ASISITIZA WATAALAMU WA HALI YA HEWA KUJENGEWA UWEZO KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA WATUMIAJI WA BAHARI



*Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa WMO, Dkt. Agnes Kijazi akichangia katika mjadala kwenye mkutano wa "WMO-IOC Joint Collaborative Board" uliofanyika tarehe 16 Juni, 2020 kuhusiana na vipaumbele vya maeneo ya ushirikiano kati ya WMO na IOC.*

Dar Es Salam;

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi ameshiriki katika mkutano wa Bodi ya Mashirikiano kati ya WMO na Kamisheni ya Kimataifa ya Masuala ya Huduma za Hali ya Hewa kwa watumiaji wa Bahari "WMO-Intergovernmental Oceanographic Commission Collaborative Board (WMO-IOC JCB)" uliofanyika tarehe 16 Juni, 2020 kwa njia ya mtandao (videoconference).

Bodi hiyo ilikutana kwa lengo la kujadili vipaumbele vya maeneo ya ushirikiano yanayohitaji kujengewa uwezo, ambayo yatashughulikiwa na majopo ya kujenga uwezo ya WMO na IOC. Dkt. Kijazi ambaye ni Makamu wa Tatu wa Rais wa WMO na Mwenyekiti wa Jopo la WMO la kujenga uwezo (WMO Capacity Development Panel) alikuwa miongoni mwa wachangia mada (panelists) kutoa mwongozo kuhusiana na vipaumbele hivyo.

Akichangia katika mada hiyo Dkt. Kijazi, alisisitiza kwamba suala la kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa wanaotoa huduma kwa watumiaji wa bahari ni la umuhimu sana, kwani wataalamu hao bado hawajapewa elimu na ujuzi wa kutosha kuhusiana na mahitaji ya wadau wa bahari wanaowahudumia.

"Suala la kujenga uwezo katika masuala ya bahari lina umuhimu wa kipekee, hususan mafunzo kwa wataalamu wa hali ya hewa wanaotoa huduma kwa watumiaji wa bahari.

Hii inatokana na kwamba Taasisi nyingi za Hali ya Hewa zina vituo vya kufuatilia hali ya bahari na kutoa huduma kwa wadau, lakini wataalamu bado hawajapewa ujuzi wa kutosha kuhusiana na mahitaji ya wadau. Hivyo tunahitaji kushughulikia masuala muhimu ya kisera na kimkakati yatakayowezesha kujenga uwezo kwa wataalamu katika ngazi ya nchi", alisema Dkt. Kijazi.

Aidha, Dkt. Kijazi alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kuimarishwa kwa miundombinu ya upimaji na ufuatiliaji katika maeneo ya bahari ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu ambazo ni muhimu katika utoaji wa huduma katika sekta hii, pamoja na ushirikiano kati ya taasisi husika kuanzia ngazi ya nchi.

Bodi ya mashirikiano katika ya WMO na IOC (WMO-IOC Joint Collaborative Board) huratibu maeneo ya mashirikiano kati ya WMO na IOC, na kwa sasa pamoja na masuala mengine itashughulikia pia suala la kujenga uwezo katika maeneo ya mashirikiano. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika mkutano huo ni pamoja rasimu ya mkakati wa miaka kumi (10) wa kujenga uwezo, ambao utahusisha utaratibu wa kufanya kazi pamoja; utaratibu wa kushirikiana na washirika wengine; na uendelevu katika shughuli za kujenga uwezo.

# MSAJILI WA HAZINA AAGIZA TMA KUCHANGIA MFUKO WA SERIKALI KUPITIA UKUSANYAJI WA MAPATO



*Msajili wa Hazina Ndugu. Athumani Selemani Mbuttuka. akizungumza na washiriki wa mafunzo ya Udhibiti na Ukusanyaji wa Mapato yaliyoandaliwa mahususi kwa Menejiment ya TMA, Dodoma, Tarehe 13 Machi 2020.*

Dodoma;

Msajili wa Hazina Ndugu. Athumani Selemani Mbuttuka ameiagiza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuchangia katika mfuko wa serikali kupitia ukusanyaji wa mapato. Hayo yalizungumzwa wakati akifunga Mafunzo ya Udhibiti na Ukusanyaji wa Mapato yaliyoandaliwa mahususi kwa Menejiment ya TMA, Dodoma, Tarehe 13 Machi 2020.

"Kupitia Ofisi yangu tutaendelea kuwasaidia na kuwapa ushirikiano katika kutimiza majukumu yenu mapya mliyokasimiwa kisheria. Aidha, nawakumbusha jukumu kubwa la kuongeza mapato na kuchangia katika mfuko wa serikali". Alisema Bw. Mbuttuka

Aliendelea kusisitiza kuwa, ujuzi uliopatikana utumike vizuri ili kusimamia vizuri zaidi jukumu jipya la udhibiti ambalo ni la kisheria pamoja na kuboresha majukumu ambayo TMA ilikuwa nayo kabla ya kuwa Mamlaka.

"Nipende kurudia tena kuwa, pale mtakapohitaji ushauri kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina msisite kuja kwani lengo letu ni pamoja na kujenga Tanzania ya viwanda na kukuza uchumi wetu ili kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 ambapo TMA ina mchango mkubwa". Alisisitiza Msajili wa Hazina.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi alisema kuwa mafunzo yameongeza morali ya kuendelea kuboresha huduma za hali ya hewa hapa nchini ili kukidhi mahitaji ya wadau kote nchini na pia yametoa uelewa wa kutosha katika eneo la kudhibiti na kuongeza mapato.

"Napenda nikuahidi mheshimiwa mgeni rasmi kwamba tutayaweka



*Mkurugenzi Mkuu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi akiwasilisha maelezo ya awali wakati wa mafunzo ya Udhibiti na Ukusanyaji wa Mapato yaliyoandaliwa mahususi kwa Menejiment ya TMA, Dodoma, Tarehe 13 Machi 2020.*


mafunzo haya katika matendo na kuisimamia vyema sheria iliyoanzisha TMA ili kuhakikisha wote wanaotumia huduma za hali ya hewa kibiashara wanachangia huduma hizo".Alieleza Dkt. Kijazi.

Aliendelea kufafanua mafunzo yaliyofanyika yameongeza uelewa kwa Menejiment ya Mamlaka ya Hali ya Hewa kuhusu jukumu jipya walilopatiwa la kudhibiti huduma za hali ya hewa hapa nchini.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA), Ndugu, Charles Senkondo alifurahishwa na jinsi washiriki hao ambao ni viongozi kutoka TMA walivyoonesha kunufaika na mafunzo hayo ambapo ndiyo dhumuni la TaGLA kusikia hivyo na si vinginevyo.

Awali, Mwezeshaji kutoka Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) Ndugu, Felix Ngamlagosi alieleza namna washiriki hao walivyoonesha dhamira (commitment) na ushirikiano wa hali ya juu katika kuhakikisha wanafikia lengo la mafunzo hayo

Mafunzo hayo ya siku tano yaliandaliwa na TMA kwa kushirikiana na TaGLA, yamejumuisha viongozi kutoka katika ofisi za TMA zilizoko kwenye kanda nane za Mamlaka ikiwa pamoja na Ofisi ya Zanzibar.




# Maswali na majibu


## Kupatwa kwa jua ni nini?

Hali ya kupatwa kwa Jua ni tukio linalohusisha kivuli cha mwezi kuangukia juu ya uso wa Dunia ambapo katika maeneo yaliyo ndani ya kivuli hicho, Jua huonekana likifunikwa na Mwezi kwa kipindi cha saa chache.

Kuna aina mbili za kupatwa kwa Jua;

i. Kupatwa kwa Jua kikamilifu ambapo mwezi huzuia kabisa mwanga wa Jua kufika katika Dunia.

ii. Kupatwa kwa Jua kipete, Mwezi huzuia sehemu tu ya mwanga wa Jua, hivyo kutengeneza umbo la pete ya mwanga wa jua angani.




*Mpangilio wa jua, mwezi na dunia unavyokuwa kipindi inapotokea tukio la kupatwa na jua (Picha kwa hisani ya BBC).*

# KUPATWA KWA JUA



Dar Es Salam;

Hali ya kupatwa kwa Jua ni tukio linalohusisha kivuli cha mwezi kuangukia juu ya uso wa Dunia ambapo katika maeneo yaliyo ndani ya kivuli hicho Jua huonekana likifunikwa na Mwezi kwa kipindi cha saa chache.

Hali hii ya kupatwa kwa Jua Kipete, ilitokea siku ya Jumapili, Tarehe 21 Juni 2020 katika baadhi ya maeneo ya Bara la Afrika .Kupatwa huku kwa jua kulianzia nchi za Afrika ya Kati, kukatisha ukanda wa Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania kwa maeneo ya Dar es Salaam, Bukoba, Arusha na Dodoma na kuelekea kusini mwa rasi ya Uarabuni, kaskazini mwa bara la Hindi na kusini mwa China na hatimaye kuishia katika Bahari ya Pasifiki. Tukio hili lilianza saa 12:50 asubuhi, kufikia kilele saa 01:45 na kumalizika saa 02:50 asubuhi kwa eneo la Tanzania.

Aidha, sehemu ya Jua iliyofunikwa na Mwezi wakati wa kilele cha kupatwa kwa Jua kipete ilitofautiana baina ya eneo na eneo. Maeneo yaliyokua ndani ya njia ya kupatwa kwa Jua yaliona kupatwa kwa Jua kwa kiwango kikubwa zaidi ikilinganishwa na maeneo yaliyokua mbali zaidi na njia hii. Kwa kuwa Tanzania iliangukia katika eneo la mbali zaidi na njia hiyo, kupatwa kwa Jua kulikuwa kudogo zaidi ambapo kufunikwa kwa Jua hakukuzidi asilimia 50%.

Kuna aina mbili za kupatwa kwa Jua; kupatwa kwa Jua kikamilifu ambapo mwezi huzuia kabisa mwanga wa Jua kufika katika Dunia na aina ya pili, kupatwa kwa Jua kipete, Mwezi huzuia sehemu tu ya mwanga wa Jua, hivyo kutengeneza umbo la pete ya mwanga wa jua angani.

## HALI YA HEWA.

Kwa ujumla hakuna athari zozote kubwa zinazotokea katika mifumo ya hali ya hewa kutokana na tukio hili la kupatwa kwa Jua.

Hata hivyo, kulitokea ongezeka la muda wa baridi katika nyakati za asubuhi hususan katika maeneo ya kaskazini mwa nchi, kutokana na maeneo hayo kuwa karibu na njia ya kupatwa kwa Jua na kuchelewa kwa mwanga wa Jua ambao husababisha uwepo wa joto.

Kwa upande mwingine, uwezekano wa kuona kupatwa kwa Jua ulipungua katika baadhi ya maeneo ya kaskazini na yale ya kati mwa nchi hususan nyakati za asubuhi kutokana na hali ya mawingu ilivyokuwa.

## USHAURI.

Wananchi wanashauriwa kutoangalia Jua moja kwa moja bila kutumia vifaa vinavyoshauriwa na wataalamu ili kuepuka athari za miale ya Jua.

Mamlaka ya hali ya hewa inaendelea kufuatilia na itatoa taarifa za mabadiliko yoyote yanayoweza kujitokeza katika hali ya hewa.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TMA, 2020 wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikiwasilishwa katika baraza hilo lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TMA, 2020 wakiimba wimbo wa mshikamano " Solidarity Forever" kwa kutumia ishara ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Korona katika baraza hilo lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TMA, 2020 wakiimba wimbo wa mshikamano " Solidarity Forever" kwa kutumia ishara ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Korona katika baraza hilo lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020*



*Mfanyakazi bora wa TMA, Ndg. Kisumo Msangi kutoka kituo cha TMA - Arusha akizungumza katika Baraza la Wafanyakazi TMA, 2020 lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020*



*Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la TMA katika picha ya pamoja na mgeni Rasmi Mhe. Mhandisi. Atashasta Nditiye katika baraza hilo lililofanyika Dodoma Tarehe 16 na 17 Machi, 2020*



*Washiriki wa mafunzo ya Udhibiti na Ukusanyaji wa Mapato yaliyoandaliwa mahusus kwa Menejiment ya TMA, Dodoma, Tarehe 13 Machi 2020 katika picha ya pamoja na mgeni rasmi*

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi) Mhandisi. Leonard Chamuriho, akizungumza na Menejiment ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wakati wa mafunzo ya udhibiti na ukusanyaji wa mapato, Dodoma.*



*Menejiment ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) katika picha ya pamoja na mgeni rasmi ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi. Leonard Chamuriho wakati wa mafunzo ya udhibiti na ukusanyaji wa mapato, Dodoma.*



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya udhibiti na ukusanyaji wa mapato, Dodoma.*



*Baadhi ya wafanyakazi wa wa TMA wakifyeka kichaka katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani 2020, maeneo ya Simu 2000.*



*Muonekano wa anga muda wa jioni likiwa na rangi nyekundu au chungwa katika baadhi ya maeneo ya nchi, Tarehe 16 Aprili 2020.*



*Muonekano wa anga muda wa jioni likiwa na rangi nyekundu au chungwa katika baadhi ya maeneo ya nchi, Tarehe 16 Aprili 2020.*

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi akisisitiza jambo wakati bodi hiyo ilipotembelea kituo cha hali ya hewa TMA - Mtwara.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt. Buruhani Nyenzi akipokea taarifa ya Kanda ya Kusini kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Kusini TMA, Ndugu Amasi Daudi.*




*Wajumbe wa Bodi ya TMA wakipata maelezo ya namna ya kifaa cha kupima mnunurisho wa jua kinavyofanya kazi.*



*Wajumbe wa Bodi ya TMA katika picha ya pamoja walipotembelea ofisi ya TMA Kanda ya Kusini-Mtwara.*



*Wajumbe wa Bodi ya TMA katika picha ya pamoja katika ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Rada ya hali ya hewa - Mtwara.*



*Wajumbe wa Bodi ya TMA katika picha ya pamoja wakiwa na baadhi ya Wafanyakazi wa TMA na Wakandarasi wa mradi wa Rada ya hali ya hewa - Mtwara.*